
JARIDA LA ROBO MWAKA LA MPANGO WA TAIFA WA

# KIFUA KIKUU

## NA UKOMA



Septemba 2023




# MAAMBUKIZI MAPYA YA KIFUA KIKUU YAPUNGUA NCHINI TANZANIA

**Dar Es Salaam**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameishukuru Serikali ya Marekani kwa jitihada zake katika kuisaidia Serikali ya Tanzania hususani katika Sekta ya Afya dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwemo Kifua Kikuu. Hayo yamesemwa wakati wa mazungumzo ya moja kwa moja baina ya Mhe. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais wa Marekani Mhe. Kamala Harris katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ukumbi wa Kikwete, Ikulu jijini Dar es Salaam tarehe 30 Machi, 2023.

"Maambukizi mapya ya kifua kikuu yamepungua kutoka Watu 306 kati ya kila Watu Laki 1 hadi Watu 208 kwa kila Watu Laki 1, Wanawake Wajawazito wenve virusi vya UKIMWI sasa wana uhakika wa kuzaa watoto wasio na UKIMWI na hizi ni jitihada za PEPFAR tunawashukuru sana" amesema Rais Samia.

Pia, kwa upande wa Mhe. Kamala Harris aliipongeza serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa na mikakati thabiti ya kutokomeza magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria.



# RAIS SAMIA AOMBWA KUWA KIONGOZI KINARA WA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA TB

**Geneva, Uswisi**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameombwa kuwa miongoni mwa viongozi kinara katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu Duniani kufuatia utekelezaji bora wa afua zinazolenga kutokomeza ugonjwa huo hadi ifikapo 2030.

Ombi hilo limetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Stop TB Partinership Dkt Lucica Ditiu, yenye makao Makuu yake mjini Geneva Uswisi wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu.

Awali akizungumza Waziri Ummy amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya Tanzania imepiga hatua katika kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu kutoka asilimia 49 mwaka 2016 hadi asilimia 65 mwaka 2022 na kusogeza huduma za uchunguzi wa Kifua Kikuu na tiba karibu na wananchi.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania imepiga hatua katika ugunduzi wa wagonjwa wapya wa Kifua kikuu hususani kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile migodini.

"Mwezi Machi mwaka huu Serikali ilizindua Mpango unaoshirikisha sekta nyingine ili kuongeza kasi ya kutokomeza Kifua Kikuu kupitia sekta hizo kuweka kipaumbele katika masuala ya ugonjwa huo", ameeleza Waziri Ummy.

Waziri Ummy amemuahidi Dkt Ditiu kuwa atafikisha maombi hayo kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa yeye binafsi amekuwa mstari wa mbele nchini katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu.

Lakini pia amesisitiza Tanzania itaendelea kuimarisha ushirikiano na Stop TB partnership ili kuhakikisha ugonjwa wa Kifua Kikuu unatokomezwa kupitia utekelezaji wa miongozo na makubaliano ya kimataifa na kikanda

kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Stop TB Partinership Dkt Lucica Ditiu ameipongeza Tanzania kwa kupunguza maambukizi mapya na vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu.

Vile vile Dkt. Ditiu ametoa wito kwa Tanzania iwe moja ya nchi kinara barani Afrika katika jukwaa la Viongozi wakuu wa nchi 10 duniani wenye lengo la kutokomeza Ugonjwa huo ifikapo 2030.

Hata hivyo amesema wito huo umetokana na Tanzania kuonyesha ubunifu katika utoaji wa huduma za kinga na tiba pamoja na kufikia malengo ya viashiria vya kutokomeza ugonjwa huo.



**"Nchi saba vinara kwa sasa ni pamoja na India, Indonesia, Philippines, Africa Kusini,**

# MAAGIZO TISA ALIYOTOA MHE. WAZIRI MKUU WAKATI WA UZINDUZI WA MPANGO WA KISEKTA WA UWAJIBIKAJI WA PAMOJA WA MAPAMBANO DHIDI YA KIFUA KIKUU NCHINI.



**1** Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali ziweke Shughuli za Kifua Kikuu katika mipango kazi yao ili kuwafikia wananchi ambao ni walengwa

**2** Mikakati yote kuhusu maswala ya UKIMWI lazima ijumuishe swala la Kifua Kikuu.

**3** Wizara ya Afya na TAMISEMI iboreshe mifumo na kuimarisha idara zake katika kutambua, kusajili na kuratibu waganga wa tiba asili ili waweze kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu na kuwaleta kwenye huduma za Afya.

**4** Wizara, idara na Taasisi zote ziandae mpango wa kufuatilia na kutathmini wenye malengo sanjari na mkakati wa Dunia wakutokomeza Kifua Kikuu nchini kufikia 2030. Mkakati huo ufanyiwe kazi na ufuatiliaji wa kila siku ufanyike, na tathmini kila baada ya miezi sita ifanyike kuona maendeleo yake.

**5** Katika kuratibu maswala ya Kifua Kikuu na huduma zingine za Afya, tuhakikishe tunaimarisha ushiriki zaidi wa wadau kutoka Sekta binafsi na asasi za kiraia na za watu binafsi na tuone zikifanya kazi ili kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu Nchini.

**6** Wizara ya Madini ipange na kutekeleza mikakati ya kudhibiti vumbi ili wachimbaji wadogo wasiambukizwe Kifua Kikuu.

**7** Sekta ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Mambo ya Ndani zishauri kuhusu makazi bora na kuboresha maeneo ya kazi ili kupunguza uwezekano wa maambukizi ya Kifua Kikuu.

**8** Halmashauri zitenge maeneo ya wazi ya wananchi ya kupumzikia katika miji pamoja na kuandaa maeneo ya michezo na burudani ili jamii ipate hewa safi

**9** Viongozi wa Wizara kukutana na kukubaliana ili kushauri namna bora ya utekelezaji wa Mkakati wa Uwajibikaji wa Pamoja wa Kisekta wa Mapambano (MAF-TB) ya Kifua Kikuu nchini.



# MAAMBUKIZI NA VIFO VITOKANAVYO NA UGONJWA WA KIFUA KIKUU VIMEPUNGUA NCHINI TANZANIA

**Simiyu, Bariadi**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa amesema kuwa vifo vinavyosababishwa na Kifua Kikuu vimepungua kutoka vifo 55,000 vilivyotokea mwaka 2015 hadi vifo 25,800 sawa na asilimia 55% kwa Tanzania.Hayo ameyasema leo Machi 24, 2023 kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) za mwaka 2022 kwenye Maadhimisho Siku ya Kifua Kikuu Duniani ambapo Kitaifa yamefanyika katika Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu.

"Halikadhalika tumepunguza maambukizi mapya ya Kifua Kikuu kutoka kiwango cha wagonjwa 306 katika kila idadi ya watu 100,000 kufikia wagonjwa 208 katika kila watu 100,000 ikiwa ni sawa na punguzo la asilimia 32." amesema Waziri Mkuu Majaliwa

Aidha, Waziri Mkuu Majaliwa amebainisha kuwa ugonjwa wa Kifua Kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria ambao unaambukizwa kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa wa Kifua Kikuu ambaye hajaanza matibabu kwenda kwa mtu mwingine.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 duniani zenye maambukizi makubwa ya ugonjwa wa Kifua Kikuu ambazo kwa pamoja zinachangia asilimia 87 ya wagonjwa wote duniani." amesema Waziri Mkuu Majaliwa

Hata hivyo, WazIri Mkuu Majaliwa amesema ifahamike kuwa Kifua Kikuu ni ugonjwa mtambuka ambao sekta ya afya pekee haitoshi kutokomeza, hivyo ni budi kuweka mkakati wa kitaifa utakaowezesha ushiriki wa sekta nyingine katika kutokomeza Kifua Kikuu ifikapo mwaka 2030. Kwa upande wake Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amesema kuwa waathirika zaidi wa ugonjwa wa Kifua Kikuu ni watu wa hali ya kipato cha chini.

# TANZANIA MWENYEJI WA MKUTANO WA KIKANDA WA AFRIKA WA MASUALA YA KIFUA KIKUU

**Arusha**

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia wa kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund ATM), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la STOP TB Partnership ulifanya mkutano wa Kikanda ya Afrika wa masuala ya Kifua Kikuu katika hoteli ya Mount Meru jijini Arusha. Mkutano huo ulishirikisha washiriki zaidi ya 70 kutoka jumla ya nchi 21 Barani Afrika na nje ya Afrika.



Washiriki wa mkutano huo muhimu walikuwa Makatibu Wakuu wa Wizara ya Afya na Mameneja Mpango wa Programu za Kifua Kikuu kutoka nchi 15 barani Afrika. Mkutano huo pia ulilenga kubadilishana uzoefu wa Makatibu Wakuu katika kuchochea kasi ya kutafuta rasimali na utashi wa kisiasa katika kupambana na Kifua Kikuu barani Afrika, kubaini changamoto na vikwazo vinavyochelewesha kufikia malengo ya kutokomeza Kifua Kikuu Duniani ifikapo 2030, kubadilishana uzoefu wa afua bora za Kifua Kikuu (TB best practices) miongoni mwa nchi za Afrika pamoja na maandalizi ya Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa Masuala ya Kifua Kikuu (UN High Level Meeting) ambao unategemewa kufanya mwanzoni mwa mwezi septemba jijini New York Marekani.



Akifungua mkutano huo Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alibainisha kuwa takwimu zinaonyesha takribani watu milioni 10 duniani huambukizwa Kifua Kikuu kila mwaka na kati ya hao watu milioni 1.6 hufariki dunia kutokana na TB pamoja na watu takribani 132,000 huambukizwa ugonjwa huo nchini Tanzania na watu 25,800 hufariki dunia kila mwaka ambapo ni sawa na wastani wa watu 70 kupoteza maisha kila siku kutokana na ugonjwa huo

“kila mwaka watu 132,000 huambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu nchini Tanzania, watu 25,800 hufariki dunia kila mwaka ambapo ni sawa na watu 70 hufariki kila siku kutokana na ugonjwa wa TB nchini Tanzania”. Alisema Waziri Ummy

Aidha, alibainisha kuwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipanga kwa kila halmashauri nchini kuendelea kushirikisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii, waganga wa tiba asili pamoja na wauzaji wa maduka ya dawa baridi ili kuongeza kasi ya uibuaji wa wagonjwa wa TB sambamba na watu waliowahi kuugua TB na kupona katika kuongeza uhamasishaji na uelimashaji wa ugonjwa wa TB kwa jamii.

Kwa upande wa mkuu wa mambo ya Kifua Kikuu kwenye mpango wa Dunia wa kupambana na magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria Dkt. Eliud Wandwa



**Mhe. Ummy Mwalimu**
**WAZIRI WA AFYA**




**Dkt. Eliud Wandwalo**

**MKUU WA MAMBO YA KIFUA KIKUU KWENYE MPANGO WA DUNIA WA KUPAMBANA NA MAGONJWA YA UKIMWI, KIFUA KIKUU NA MALARIA**

lo alibainisha sababu iliyopelekea mkutano huo kufanyika nchini Tanzania na si nchi zingene barani afrika,

“Tumechagua Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huu kwa sababu imekuwa na mafanikio makubwa kwenye mapambano dhidi ya Kfua Kikuu miongoni mwa nchi zingine za Afrika.

Kwa takwimu toka WHO inaonyesha kuna nchi kama tano barani Afrika na nchi chache barani ulaya zimepiga hatua katika kufikia malengo ya kidunia ya kutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu ambapo Tanzania imeyafikia malengo hayo” alisema Dkt. Wandwalo.

Dkt Wandwalo aliongeza kwa kusema Mfuko wa Dunia utaendelea kusaidia jitihada za kutokomeza ugonjwa wa TB nchini Tanzania na duniani kwa ujumla mpaka pale ugonjwa huu utakapotokomezwa kabisa pindi ifikapo mwaka 2030 pamoja na kutenga kiasi ya dola bilioni 2.4 kwa ajili ya kusaidia nchi zote kwa kipindi cha miaka 3 ijayo zenye tatizo la ugonjwa wa Kifua Kikuu duniani na Tanzania ikiwemo.




# DKT MOLLEL ABAINISHA MIKAKATI YA KUTOKOMEZA UGONJWA WA UKOMA NCHINI TANZANIA IFIKAPO 2030

**Dodoma**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel amesema, Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuchukua hatua muhimu ili kufikia malengo ya utokomezaji wa Ukoma katika Taifa letu na tayari imetengeneza mikakati ya kufikia visa sifuri vya Ukoma ifikapo mwaka 2030. Amesema hayo wakati akitoa tamko la maadhimisho ya siku ya Ukoma Duniani yenye kauli mbiu ya "Chukua hatua sasa, tokomeza Ukoma nchini." Amesema, miongoni mwa hatua Wizara ilizochukua ni pamoja na;

- Kutoa mafunzo elekezi kwa watoa huduma hasa katika maeneo ambayo Ukoma bado ni tatizo kubwa.
- Kujumuisha utokomezaji Ukoma na afua zingine za afya katika ngazi za Mikoa na Halmashauri
- Kubaini na kufanya uchunguzi wa Ukoma katika kaya zote zenye wagonjwa wa Ukoma.
- Kuhakikisha wagonjwa wote wapya wanaoibuliwa wanapatiwa matibabu husika bila kukosa.
- Kuongeza kasi ya uelimishaji jamii na ushiriki wake katika mapambano.
- Kupanua wigo wa utoaji wa Tibakinga ya Ukoma na kuyafikia makundi yote katika taifa zima.
- Kuongeza uwezo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa Ukoma katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini.
- Kuendeleza juhudi za kufanya tafiti na kuibua mbinu bunifu za kuharakisha kasi ya utokomezaji.
- Kuboresha matunzo na huduma kwa watu wenye ulemavu utokanao na Ukoma.
- Kuongeza kasi ya elimu kwa umma na kukomesha vitendo vyote vyenye sura ya unyanyapaa na ubaguzi dhidi ya wanaougua na watu walioapata athari za Ukoma.

# WIZARA YA AFYA YAZINDUA ZOEZI LA MAPITIO YA KATI YA MPANGO MKAKATI WA SITA WA KIFUA KIKUU NA UKOMA 2020-2025

**Dodoma**

Wizara ya Afya kupitia Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma imezindua zoezi la mapitio ya kati ya Mpango Mkakati wa Sita (NSP VI 2020-2025) wa Kifua Kikuu na Ukoma. Uzinduzi wa zoezi hilo umetekelezwa na Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Samuel Lazaro leo tarehe 30 Januari, 2023 katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.

Matokeo ya tathmini hii yatasaidia kuboresha Mpango Mkakati wa VI katika kipindi cha muda wa utekelezaji uliobaki wa mwaka 2023-2025 na hivyo kufikia malengo ya kitaifa na kidunia katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma.

Aidha, tathmini hii itasaidia pia Kutoa dira katika uandishi wa maombi ya awamu ya nne ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia (NFM4) na Mkakati wa USAID Global TB.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Watathmini wa nje kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), USAID,Stop TB partnership, Watalaam Washauri Wabobezi wa Kimataifa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Afya pamoja na wadau mbalimbali wa utekelezaji wa afua za Kifua Kikuu nchini.

Ziara ya tathmini hiyo inaanza kufanyika leo tarehe 30 Januari,2023 mpaka tarehe 05 februari,2023 katika mikoa 14 nchini iliyopendekezwa.





# KIBONG'OTO SHIRIKIANENI NA MKUTA KUTENGENEZA MPANGO KAZI WA MATOKEO YA UTAFITI KWA WALIOWAHI KUUGUA TB NA KUPONA.

**Dodoma**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumain Nagu ameitaka Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibongóto kwa kushirikiana na Mtandao wa Watu Waliougua Kifua Kikuu na Kupona (MKUTA) kuhakikisha wanakuja na mpango kazi wa kufanyia kazi matokeo ya utafiti wa mwaka mmoja uliofanyika wa kuchunguza watu waliowahi kuugua kifua kikuu na kupona lakini baada ya kupona hawakufatiliwa kwa karibu.

Prof. Nagu ametoa wito huo leo jijini Dodoma katika ufunguzi wa kikao kazi cha usambazaji wa matokeo ya mwaka mmoja ambao umeweza kushirikisha watu waliowahi kuumwa Kifua Kikuu na kupona lakini baada ya kupona wakawa hawafatiliwi kwa karibu kujua maendeleo yao. Prof. Nagu amesema kuwa wanatakiwa kuwasilisha mpango kazi kwa wizara kulingana na matokeo waliyopata kutoka katika utafiti uliofanyika ili kuhakikisha wanaongeza umakini dhidi ya maambukizi ya Kifua Kikuu nchini.

Naye Mkurungenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto iliyopo Wilaya ya Siha Mkoa wa Kilimanjaro Dkt.Leonard Subi amesema kuwa kupitia utafiti huo wameweza kupata zaidi ya watu 625 ambao walikuwa katika jamii na watu hao wamefanyiwa uchunguzi tena kuona kama hawana Kifua Kikuu.

“Katika watu 625 tulio wafanyia uchunguzi tumeweza kugundua asilimia 24 kati yao tayari walishaugua tena Kifua Kikuu na wapo katika jamii na watu nane walikuwa ni wale waliopona Kifua Kikuu sugu”, ameeleza Dkt. Subi

Hivyo ametoa rai kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kushirikisha jamii hususani katika kuwafatilia kwa ukaribu watu waliougua Kifua Kikuu na kupona ili kujua maendeleo yao katika jamii.



**Dkt. Leonard Subi**
MKURUNGENZI MTENDAJI WA HOSPITALI YA TAIFA YA MAGONJWA AMBUKIZI YA KIBONGÓTO

# SERIKALI KUENDELEA KUSHIRIKIANA NA WADAU KUTOKOMEZA UGONJWA WA KIFUA KIKUU NCHINI.



**Dodoma**

Serikali imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau katika sekta zote ili kudhibiti na kuutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB) ifikapo mwaka 2030. Hayo yamesemwa leo na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim Yonazi kwenye kikao na Makatibu Wakuu wa Wizara kilichofanyika katika ofisi za Waziri Mkuu Jijini Dodoma.

"Ili kudhibiti ugonjwa huu wa Kifua Kikuu ni muhimu kushirikiana na wadau wengi kama sekta ya afya, sekta ya elimu, sekta ya usafirishaji na sekta nyingine mbalimbali." amesema Dkt. Yonazi Kwa upande wake Mtaalamu Mshauri kutoka Stop Tb Partnership (STP) Bw. Oscar Mukasa wakati akiwasilisha taarifa ya mpango kazi wa kudhibiti Kifua Kikuu amesema watu wenye hatari zaidi yakupata Kifua Kikuu ni pamoja na watu wanaoishi kwenye makazi duni, Watoto, Wavuvi na wanafunzi wanaoishi katika shule za Bweni.

Pia, amesema Watu wenye VVU, watu wenye Utapiamlo, wachimbaji madini, wanaoishi na mgonjwa wa Kifua Kikuu, watoa huduma za afya na wanaotumia madawa ya kulevya kwa kujidunga sindano.

Mwisho, Bw. Mukasa amewashauri wanaoishi katika mazingira hayo kuchukua tadhari za kujikinga na ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB).



# WATAALAMU WA AFYA ZAIDI YA 100 WAPATIWA MAFUNZO NAMNA YA KUJAZA TAARIFA ZA DAWA ZA KIFUA KIKUU NA UKOMA KWA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA KUPITIA MFUMO WA KIELETRONIKI WA eLMIS.

**Arusha**

Wataalamu wa afya zaidi ya 100 kutoka Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Singida wapatiwa mafunzo kuhusu namna ya kujaza taarifa za dawa za Kifua Kikuu na Ukoma kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kupitia mfumo wa kieletroniki wa eLMIS. Wataalamu hao ni Wafamasia wa Mikoa, Wilaya na Hospitali, Waratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma wa Mikoa na Wilaya pamoja na Waratibu wa Maabara wa Mikoa. Mafunzo hayo yamefanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uhasibu jijini Arusha.

Akifungua mafunzo hayo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Slyvia Mamkwe, amewataka wataalamu hao kutumia mafunzo hayo kuboresha mnyororo wa namna ya kuagiza na kujaza taarifa za dawa za Kifua Kikuu na Ukoma katika Mikoa yao. Vilevile amewataka wataalamu hao Kwenda kuwafundisha watoa huduma za afya katika Mikoa wanayotoka ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria mafunzo hayo muhimu.

"Nina imani kila mmoja wetu akitoka katika mafunzo haya ataenda kuwafundisha watoa huduma za afya katika vituo husika ili kuwajengea uwezo wa namna ya - uagizaji na ujazaji taarifa za dawa za Kifua Kikuu na Ukoma kwa njia ya kieletroniki" alisema Dkt. Slyvia Aidha Dkt. Slyvia aliwasisitiza wataalamu hao pindi wanapoomba dawa zote ni lazima watumie mfumo huo wa kieletroniki sambamba na kutuma ripoti kwa wakati ili kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Nae muwezeshaji mkuu wa mafunzo hayo kutoka shirika la Global Health Supply Chain (GHSC) Bw. Vicent Manyilizu amesema mafunzo hayo yatawasaidia wataalamu hao kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kusaidia kurahisisha kutoa huduma bora kwa wananchi katika maeneo yao.






# TUONGEZE NGUVU ZAIDI KUPAMBANA NA UGONJWA WA KIFUA KIKUU ILI TUUTOKOMEZE IFIKAPO 2030

**New York USA.**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ametoa rai kwa Jumuiya za Kimataifa kushirikiana na Serikali katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa kuongeza nguvu zaidi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuweza kuutokomeza kabla ya Mwaka 2030.

Waziri Ummy amesema hayo alipokuwa akitoa tamko la Tanzania kuhusu mapambano dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwenye vikao vinavyoendelea vya Mkutano Mkuu wa 78 wa Umoja wa Mataifa.

“Bado hakuna rasilimali za kutosha kupambana na TB, tunaendelea kuhimiza wadau wa Sekta ya Afya kuunganisha nguvu za pamoja na kuwekeza zaidi kwenye rasilimali, tafiti, teknolojia, vifaa na vifaatiba” amesema Waziri Ummy.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 zenye watu wengi wenye maambukizi ya Kifua Kikuu ikichangia asilimia 87 ya ugonjwa wa Kifua Kikuu duniani.

“Takwimu za mwaka 2021 zinaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na watu 132,000 wanaogua ugonjwa wa kifua Kikuu, tumeweza kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa huu kwa asilimia 32 na vifo vitokanavyo na ugonjwa huo kwa asilimia 55” amesema Waziri Ummy na kusema kuwa Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuutokomeza ifikapo 2030.

Katika kuhakikisha ugonjwa huo unatokomea ifikapo mwaka 2030, Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania imewekeza nguvu kubwa

kwenye utoaji wa matibabu ya Kifua Kikuu pamoja na utoaji wa elimu ya afya ili jamii iweze kufahamu ugonjwa huo mapema na kupata matibabu.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inatekeleza Mpango Mkakati Shirikishi wa Sekta ya Afya katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu uliozinduliwa mwezi machi 2023 utakaosaidia kuongoza katika mapambano dhidi ya Kifua Kikuu.

Waziri Ummy amesema kuwa Tanzania inaungana na nchi nyinginezo chini ya Umoja wa Mataifa kwa kuendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo na imeridhia azimio lililowekwa la kuendelea na mapambano dhidi ya Kifua Kikuu.





# TAASISI YA SASAKAWA HEALTH FOUNDATION YA JAPAN YAAHIDI KUSHIRIKIANA NA TANZANIA KATIKA KUTOKOMEZA UGONJWA WA UKOMA NCHINI

**Dar es Salaam,**

Taasisi ya Sasakawa Health Foundation chini ya Mwavuli wa Taasisi Mama ya The Nippon Foundation ya Nchini Japan wameahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kutokomeza ugonjwa wa Ukoma kabla ya Mwaka 2030.

Hayo yamejiri Septemba 29, 2023 wakati wa kikao kifupi kati ya Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Sasakawa Health Foundation Prof. Takahiro Nanri kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Balozi wa Japan nchini Tanzania, Mhe. Yasushi Misawa.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu amewakarabisha na kumshukuru Mhe. Balozi Misawa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo kwa kuonyesha nia ya dhati katika kupambana na Ugonjwa wa Ukoma ambao umegubikwa na sifa ya unyanyapaa na kutengwa kwa wanao athiriwa na ugonjwa huo.

Aidha, Waziri Ummy amesema kuwa bado ugonjwa wa UKOMA upo nchini na Tanzania ni moja ya nchi 23 zilizobainishwa na WHO kuwa ni za kipaumbele katika kutokomeza ugonjwa wa UKOMA. Alieleza kuwa dawa za kutibu ugonjwa huu zipo na huduma zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan bila malipo kwa wagonjwa wote wenye Ukoma na mgonjwa anapona kabisa.

“Kwa kuendelea kushirikiana kwa pamoja na kuangalia maeneo ya ushirikiano tunaweza kutokomeza kabisa ugonjwa wa Ukoma ifikapo Mwaka 2030”. Amesema Waziri Ummy

Balozi Misawa amesema lengo la ziara hiyo ni kuja kuleta salaam kutoka kwa Balozi wa Dunia Mhe. Yohei Sasakawa katika kutokomeza ugonjwa wa Ukoma Duniani ikiwa ni pamoja na kuonyesha nia ya kuja nchini kupanda Mlima Kilimanjaro na kuweka bendera juu ya kilele cha Bara la Afrika ili kuhamashisha mataifa yote kuongeza kasi ya kutokomeza Ukoma barani Afrika kabla ya Mwaka 2030.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sasakawa Health Foundation Prof. Takahiro Nanri ameelezea namna ambavyo Serikali ya Japan kupitia Taasisi hiyo itakavyoweza kusaidia kutekeleza mpango wa Wizara wa kutokomeza kabisa Ukoma na madhira yake ifikapo mwaka 2030.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Kikao cha kumpitisha Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Bw. Jim James Yonazi juu ya mkakati wa Kisekta wa Kuratibu Uwajibikaji wa Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu nchini (Multi Sectorial Accountability Framework) ambao ulizinduliwa na Mhe. Waziri Mkuu siku ya maadhimisho ya Kifua Kikuu Duniani tarehe 24 Machi 2023 katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu.

Washiriki wa kikao cha kuwapitisha Wakurugenzi wa Wizara mbalimbali kwenye Mkakati wa Uwajibikaji wa kisekta katika Mapambano Dhidi ya Kifua Kikuu nchini, kikao hicho kilifanyika tarehe 23 Februari, 2023 katika ukumbi wa Mikutano Ofisi ya Waziri Mkuu Jijini Dodoma.





Kaimu Meneja Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Peter Neema akielezea mikakati mbalimbali iliyopo katika kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma nchini ifikapo mwaka 2030 mbele ya Waziri wa Afya Mhe Ummy Mwalimu pamoja na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa

# MATUKIO KATIKA PICHA




Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akishuka kutoka kwenye gari la kisasa la huduma mkoba za kliniki tembezi (Mobile Van Clinic) mara baada ya kutembelea gari hilo na kuona huduma mbalimbali za kiuchunguzi na ugunduzi wa Kifua Kikuu zitolewazo kwenye gari hilo hasa katika maeneo ambayo huduma za Kifua Kikuu ni vigumu kufikika na yenye wagonjwa wa Kifua Kikuu.

Washiriki kutoka nchi mbalimbali barani afrika wakiwa katika kikao cha pamoja waki-jadili na kubadilishana uzoefu juu ya masuala mbalimbali kuhusu ugonjwa wa Kifua Kikuu katika ukumbi wa Mount Meru jijini Arusha.





Mkuu wa Programmu na Uimarishaji Mifumo Dkt. Catherine Joachim (kati-kati) akiwa na washiriki mbalimbali kutoka nchi ttofauti tofauti barani afrika wakibadilisha uzoefu juu ya masuala mbalimbali kuhusu ugon-jwa wa Kifua Kikuu katika ukumbi wa Mount Meru jijini Arusha.




**“Tuunganishe nguvu pamoja katika kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma nchini”**